# Mwongozo wa Jamii kwa Mkakati wa Mpango Kazi wa Usawa wa Kijinsia wa Mfuko wa Kimataifa 2014-2016

eannaso

**Regional Platform**
for Communication and Coordination
on HIV/AIDS, Tuberculosis and Malaria
For Anglophone Africa

## MKUTADHA KIDOGO:

Mfuko wa Kimataifa unashughulikia mahitaji ya wale walioathirika zaidi. Ilikufikia haya, Mfuko wa Kimataifa umezindua mpango mpya wa ufadhili. Mpango huu mpya wa ufadhili unatoa fursa mpya katika utekelezaji wa mkakati wa Usawa wa Kijinsia kupitia mpango husika wa kushughulikia wale walioathirika na kuambukizwa na Ukimwi, Kifua Kikuu na malaria, kuptia pia mchakato husishi katika maombi ya nchi zinazoendelea, pamoja na kuweka msisitizo katika usimamizi wa kina katika misaada.



### *Kwa hivyo, Mkakati wa Usawa wa Kijinsia ni nini?*

Mkakati wa Usawa wa Kijinsia wa Mfuko wa Kimataifa ni sehemu ya Mkakati wa Mfuko wa Kimataifa 2012-2016: kuwekeza katika athari. Unahusisha zaidi kufikia mahitaji ya kiafya kwa wanawake na wasichana katika kukabili Ukimwi, Kifua Kikuu na malaria. Lengo zima ni kufikia, uwekezaji wa juu wa athari ambazo zinahusisha jinsia (zinazojali usawa wa kijinsia) ambazo zitaokoa maisha na kuzuia maambukizi mapya.

**NI JINSI GANI UKATILI WA KIJINSIA UNAVYOSABABISHA ONGEZEKA LA MAAMBUKIZI YA UKIMWI, KIFUA KIKUU NA MALARIA KATIKA JAMII.**

### *Msisitizo hasa ni kwa misaada ya Mfuko wa Kimataifa ushughulikie suala la kutokuwepo kwa usawa wa kijinsia.*

Mfuko wa Kimataifa unaweka msisitizo wa kiupendeleo katika kufadhili mipango ambayo inayopinga kutokuwepo kwa usawa wa kijinsia na kuimarisha mwito kwa kupigana dhidi ya magonjwa haya matatu kwa wanawake na wasichana. Mfuko wa Kimataifa utasaidia na kufadhili maombi ya misaasa ambayo:

- Kuimairisha huduma na mipango itayopunguza hathari za kijinsia na maambukizi
- Kupunguza mzigo wa maradhi kwa wale walio katika hatari kubwa zaidi
- Kupunguza athari za magonjwa hayo matatu na Kushughulikia kutokua na usawa na ubaguzi

Haki za kibinadamu

Hizi zinahimiza kwamba kijinsia ni lazima kupambana na vitendo Mwanamke vyote vinavyo mkandamiza Mwanamke anayeongoza katika jamii.

Udhibitisho wakisayansi

Vita dhidi ya ukatili wa vinamlenga zaidi kwani ndiye kwa kuwa maambukizi ya Ukimwi,Tb na Malaria

## *Baadhi ya vipaumbele vitakuwa:*

1. Kuzuia maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto
2. Kuzuia ukatili wa kijinsia na kukabili tabia potufu za kijinsia
3. Kushughulikia mahitaji ya akina mama waliokatika hatari kubwa

**KATIKA AZMA KUBWA YA KUWA NCHI ZINASHUGHULIKIA KWA UMAKINI MAHITAJI NA ULINDAJI WA HAKI ZA WANAWAKE NA WASICHANA, BAADHI YA MIPANGO ITAJUMUISHA:**

### *Kuchukua fursa za mfumo mpya wa ufadhili*

Mfumo mpya wa ufadhili unafungua fursa mpya na kuwezesha usawa wa jinsia na kushirikisha wanawake wote

### *Ushirikishaji, ushirikishaji ushirikishaji*

Utekelezaji makini wa usawa wa kijinsia hautawezekana bila ushirikiano mzuri ambao unajumuisha wadai wengi. Hawa wanajumuisha Mashirika yasiyo ya Kiserikali (NGOs) pamoja na mashirika ya kijamii

### *Uimarishaji wa mawasiliano kuhusu usawa wa kijinsia*

Jitihada na msisitizo utawekwa katika kuhakikisha mkakati wa Usawa wa Kijinsia pamoja na athari za upatikanaji pamoja na umuhimu wake kwa wadau.

**Kulingana na mipango hii, ili misaada hii iweze kusaidia mipango ya haki na uwazi, michakato fulani inahitajika kufikia ujumuishaji wa jinsia katika ngazi zote za utoaji wa misaada. Mfuko wa Kimataifa:**

Utafanya kazi kusaidia ushirikishaji wa wawakilishi wanawake pamoja na mashirika ya wanawake katika mifumo na kazi zake

Kujenga na kuendeleza ushirikishaji ili kusaidia misaada mizuri ya kijinsia

Kuimarisha uwezo wa kitaalamu wa masuala ya kijinsia kupitia uboreshaji wa mawasiliano

## MKAKATI UNA MALENGO MANNE ILI KUHAKIKISHA MISAADA YA MFUKO WA KIMATAIFA UNASHUGHULIKIA KUTOKUA NA USAWA WA KIJINSIA:

| MALENGO MADHUBUTI | HII INAMAANISHA NINI? |
|---|---|
| 1. Kuhakikisha kwamba sera za Mfuko wa Kimataifa, mipango na mifumo inasaidia mipango ambayo inashughulikia kutokua na usawa wa kijinsia | 1. Mpango wa usawa wa kijinsia unatakiwa kuwa katika msingi wa maamuzi yote. Usawa wa kijinsia ni nguzo muhimu katika mchakato wa utoaji wa misaada. |
| 2. Kuanzisha na kuimarisha ushirikishaji mzuri unaosaidia katika mipango ya utekelezaji ambayo inashughulikia kutokua na usawa pamoja na kupunguza athari kwa wanawake na watoto, kutoa usaidizi mzuri wa kitaalamu, na Kujenga uwezo wa makundi ambayo hayashiriki katika mipango ya Mfuko wa Kimtaifa ila yanayopaswa kushiriki. | 2. Washiriki wanapata usaidizi ili kuhakikisha uswa wa kijinsia ni sehemu ya ufadhili wa Mfuko wa Kimataifa. |
| 3. Kuandaa mkakati madhubuti wa mawasiliano na uenezi ambao unakuza mkakati wa Usawa wa Kijinsia na kukuza miradi kwajili ya wanawake na wasichana pamoja na wanaume na watoto. | 3. Kuhakikisha kwamba kila mtu anapata taarifa muhimu kuhusu usawa wa kijinsia. |
| 4. Kuwa na uongozi bora, ndani nan je, kwa kusaidia uenezi na kutoa sauti katika Mkakati wa Usawa wa Kijinsia. | 4. Kuhakikisha kwamba Mfuko wa Kimataifa una ujuzi mzuri na usaidizi wa kukabiliana na kutokua na usawa wa kijinsia |

## MAZINGIRA YA KIAFYA YAMESHUGHULIKIAJE SUALA LA USWA WA KIJINSIA KATIKA UKIMWI, KIFUA KIKUU NA MALARIA?

- Kuongeza jitihada katika kushughulikia ukatili wa kijinsia, kupitia Ukimwi, kama sehemu ya ajenda ya kimataifa ya jinsia
- Kuongeza jitihada kushughulikia afya ya uzazi, watoto wa changa na watoto, pamoja na uzazi wa mpango
- Kuongeza ushirikishaji wa mashirika ya kiraia katika vita dhidi ya Kifua Kikuu
- Kuongeza msisitizo kwenye kuimarisha mifumo ya kiafya ambayo inasaidia mfumo wa kimazingira na kuhakisha upatikanaji mzuri wa huduma
- Kuzindua Mpango wa Kimataifa unaosaidia kutokomeza maambukizi mapya ya Ukimwi kwa watoto ifikapo mwaka 2015 pamoja na kuhakikisha mamazao wanabaki hai.

## WASILIANA NA MPANGO WA KIKANDA

Regional Platform for Communication and Coordination for Anglophone Africa Hosted by EANNASOArusha, TanzaniaTel: +255 737 210598Email: eannaso@eannaso.org | Website: www.eannaso.org
Facebook: www.facebook.com/eannaso.org | Twitter: @eannaso